JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU

SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MASONYA

S.L.P 159.
TUNDURU
13/06/2023

NAMBA ZA SIMU.
Mkuu wa shule: **0759627804/0629868342**
Makamu wa Mkuu wa Shule: **0756903282/0625711669**/0773030446

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ..............................
.....................................................................
S.L.P ............................................................
............................................

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA MASONYA, MWAKA 2023/2024**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha TANO (V) katika shule ya Sekondari ya wasichana Masonya kidato cha TANO 2023/2024 tahasusi ya.............
Aidha kwa niaba ya jumuiya ya shule ya sekondari ya WASICHANA MASONYA natumia nafasi hii kukupongeza kwa kuchaguliwa na karibu sana shule ya Sekondari ya Wasichana Masonya.

Shule ya sekondari ya wasichana Masonya ni shule ya BWENI, na ipo umbali wa kilometa kumi na mbili (12) kaskazini mwa mji wa TUNDURU. Kilometa sita (06) ukitoka Tunduru mjini kuelekea barabara kuu iendayo Songea, upande wa kulia utaona kibao kinachoonyesha shule iliko. Kutoka kwenye kibao hicho ni umbali wa kilometa sita (06) mpaka shuleni.

Usafiri wa kutoka Stendi kuu ya mabasi yaendayo mikoani unapatikana, nje ya stand kuna maegesho ya Taxi, bajaji pamoja na pikipiki kwa gharama zifuatazo: Taxi mpaka shule 10000/= Mchana na 15000/= (usiku), Bajaji 6000-8000/= (Kukodi) na 1500-2000 kama abiria wa kawaida na pikipiki 3000-5000/= mpaka shuleni. Kila mwanafunzi anajitegemea kwa safari zote za kuja shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo au dharura yoyote ile.

Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13/08/2023 mwisho wa kuripoti ni tarehe /08/2023 (ama muda utakao pangwa na kutangazwa na OR-TAMISEMI)
Mwanafunzi akichelewa kuripoti ndani ya kipindi hicho nafasi yake itajazwa na mwanafunzi mwingine.

**Tafadhari kama umepata shule sehemu nyingine na hutaripoti, tutumie taarifa kwa barua ili Wizara impe nafasi hiyo mwanafunzi mwingine mapema iwezekanavyo.**

Pamoja na barua hii nimeambatanisha fomu mbalimbali na maelekezo muhimu kama ifuatavyo:
1. Maelekezo ya mambo muhimu ya kuzingatia

2. Fomu ya kupimwa afya (Medical examination report form) vipimo vifanyike kwenye hospitali za selikali, hakikisha unapimwa na sio kujaziwa fomu tu, mwelekeze Mganga matatizo ya Afya uliyonayo kwani hatutapokea hoja zozote za ugonjwa kinyume na ripoti ya Mganga.

3. Fomu ya kukubali nafasi ya kujiunga, ahadi ya mwanafunzi kufuata sheria na kanuni za shule pamoja na ahadi ya mzazi /mlezi kuonyesha ushirikiano kwa shule ikiwemo kulipa michango ya shule.

4. Fomu ya taarifa binafsi za mwanafunzi
Kumbuka kuwa kila mwanafunzi anapaswa kujaza fomu zote husika kwa ukamilifu na kuzirejesha hapa shuleni siku atakaporipoti. M**OTTO NI ELIMU NIDHAMU NA MICHEZO.**

**KARIBU SANA MASONYA SEKONDARI**

……………………………………………………

**MAKRINA T. NGONYANI**
**MKUU WA SHULE**

THE HEADMISTRESS
MASONYA GIRLS S.S
BOX 159
TUNDURU

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**1. 1 Sare ya shule**

(a) Sketi mbili (02) za rangi ya kijivu ya kupauka (Kitambaa cha suti) ndefu zinazokaribia usawa wa kisigino mshono wa linda boksi.

(b) Gauni mbili (02) za kazi (shamba dress) rangi ya bluu (sio blue bahari au dark blue) , ziwe ndefu zinazokaribia usawa wa kisigino mshono solo mikono mifupi (Kitambaa aina ya polista).

(c) Tai mbili (2) za rangi ya kijivu.

(d) Shati mbili (2) nyeupe mikono mirefu aina TOMATO.

(e) Viatu vya ngozi rangi nyeusi vya kamba (jozi mbili)

(f) Soksi nyeupe ndefu (stockings) jozi zisizo pungua mbili (2)

(g) Sweta moja ama zaidi rangi ya kijivu (iwe na rangi moja tu)

(h)Unaruhusiwa kushona **HIJAB** kwa anayetaka, na inatakiwa ishonwe ama ifuatavyo:

(i) Nusu kanzu inayofunika makalio, isiyobana, yenye mikono mirefu na hijabu ishonwe ifunike viganja vya mikono.(isiwe ndogo yenye marembo) rangi nyeupe kitambaa aina ya HALUWA na sio aina ya MPIRA.

(ii) Sketi iwe ndefu kama ilivyoelekezwa hapo juu (**a**)

(iii) Kwa anae vaa HIJAB gauni la kazi (shamba dress) liwe la mikono mirefu na vigezo vingine kama vilivoelekezwa kwenye (**b**).

(iv) HIJAB rangi ya bluu itakayovaliwa na gauni wakati wa kazi za nje. (kitambaa kama cha gauni na sio cha mpira) na ishonwe kwa kufuata maelekezo ya Hijabu katika (i) hapo juu.

(i) Trakisuti moja ya rangi ya bluu bahari (Light blue na sio blue au dark blue) kwa ajili ya kuzuia mbu wakati wa usiku(**isiyobana**).

(j) Nguo za ndani za kutosha.

(k) Tshirt ya shule (zinapatikana shuleni)

**NB.Mwanafunzi HARUHUSIWI kuja na nguo za nyumbani isipokuwa sare alizoelekezwa, na mwanafunzi aje akiwa amevaa sare za shule na sio vinginevyo.**

**2.1 Sare za michezo.**

**(i)**Jezi ya Timu ya Taifa ya tanzania moja (rangi ya bluu tshirt na bukta yake)

(ii) Raba jozi moja (Rangi nyeusi)

(iii) Sketi fupi rangi ya bluu ( Kwa anayetaka ishonwe kama ilivyo sketi ya netball)

**3.1 Mahitaji ya darasani**

(i) File moja kwa ajili ya kutunzia mitihani yake (spring file za plastiki) rangi ya bluu.

(ii) Daftari zisizopungua saba (COUNTER BOOKS )ukubwa zisipungue quire 03,mkebe,rula na vifaa vingine vya kuandikia kama vile kalamu (wino na risasi) pamoja na begi la kubebea daftari.

(iii) Scientific calculators (isiyo programmable) fx-991 MS kwa wanaosoma HGK na HGL

(iv) Vitabu mbalimbali kulingana na masomo anayosoma.

**4.1 Vifaa vingine muhimu ambavyo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni.**

(i) Ream mbili (02) za karatasi kwa mwaka A4 kwa ajili ya "Photocopy"

(ii) Godoro moja lenye ukubwa wa Ft 2½ kwa 6.

(iii) Shuka mbili (2) rangi ya blue na blanketi moja na chandarua (rangi nyeupe).

(iv) Vyombo vya chakula (alete container na kikombe rangi ya bluu, pamoja na kijiko).

(v) Ndoo ndogo mbili zenye mifuniko (rangi ya blue).

(vi) Sanduku la bati kwa ajili ya kuwekea nguo na vifaa vingine.

(vii)Taulo, kitenge doti moja na ndala kwa ajili ya kuogea.

(viii) Picha mbili za passport size (background ya bluu bahari)

(ix) Tochi kwa ajili ya matumizi ya usiku atokapo bwenini kwenda darasani.

**Vifaa vya usafi**

(x)Fagio la plastiki laini moja (Soft broom)

(xi)Fagio la plastiki gumu (Hard broom)

(xii) Sabuni ya chooni lita tano (05)

(xiii)Fagio la kusukumia maji la mpira(drier) moja na brash ngumu yenye mpini mfupi wa mbao kwa ajili ya kusafishia sinki la choo.

**5.1 MICHANGO YA SHULE**

(i) Shilingi 65,000/= kwa ajili ya uendeshaji wa shule.
(ii) Shilingi 5,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha (aje nayo)
(iii) Fedha ya tahadhari (caution money) 5,000/= (haitarejeshwa).
(iv) Shilingi 5,000/= kwa ajili ya Nembo

NB. Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na kadi ya BIMA ya AFYA kwa ajili ya matibabu anapokuwa mgonjwa au anashauriwa aje na Tsh50400/= (Mkononi) kwa ajili ya kujiunga na Bima kwa ajili ya wanafunzi.

**Michango ilipwe NMB kwenye akaunti ya shule Na. 70901100056- jina la akaunti ni SHULE YA SEKONDARI MASONYA kama ilivyoelekezwa hapo juu kwenye 5.1 (i).**
**-Tafadhari andika majina sahihi ya mwanafunzi kwenye pay slip na Mwanafunzi leta nakala halisi ya PAY SLIP.**

**6.1. CHAKULA**

Shule inatoa huduma ya chakula ambacho huliwa na watanzania wote ambacho selikali inapendekeza kuliwa na wanafunzi. Endapo mwanafunzi ana miiko ya kutokula vyakula furani, tafadhari usiipokee hii nafasi kwani shule haitatoa huduma pekee kwa kila mwanafunzi. Pia shule haitoi kibali cha kwa mwanafunzi kujipikia hivyo asilete chakula chochote kile wala kinywaji cha aina yeyote, na haturuhusu mwanafunzi kununua aina yoyote ya chakula/vinywaji toka nje ya shule.

**7.1. SHERIA ZA SHULE.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu na 25 ya mwaka 1978, na kama ilivyoboreshwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inaingatia miongozo yote inayotolewa na wizara Elimu sayansi teknolojia na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya Elimu Nchini na Ofisi ya RAIS-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Zifuatazo ni sheria na kanuni za shule ambazo mwanafunzi anatakiwa azifuate.

**(A)SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

i. Kusimama na kumsalimu mwalimu au mtu yeyote aliyewazidi umri anapopita, anapoingia darasani ama ukumbi wa mikutano.
ii. Mwanafunzi awaheshimu wafanyakazi wote walioko shuleni kama walezi wake, kushirikiana na wanafunzi wenzake katika kazi na kutotumia lugha chafu kwa mtu yeyote yule.
iii. Mwanafunzi awe na kucha Fupi zisizo pakwa rangi, nywele fupi wakati wote, urefu unaowezesha kijiti cha kiberiti kuonekana, hairuhusiwi kunyoa kipara au mitindo mingine kama vile kiduku, kijoti, kiseveni nk.
iv. Kuheshimu na kukubali tofauti za kisiasa, kidini na kiutamaduni zilizopo katiaka jamii
v. Kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote upewazo shule na kushiriki kikamilifu.
vi. Mwanafunzi ni lazima awe katika mavazi Rasmi ya shule siku zote za masomo(Mda wote wa vipindi), anapotoka nje ya shule kwenda hospitali au katika shughuli yeyote ya kishule, mwanafunzi anaposafiri kuja shuleni au kwenda kwao wakati wa likizo.
vii. Ni kosa kwa mwanafunzi kupita njia zisizo rasmi,kutupa takataka maeneo yasiyo rasmi au kuziona taka bila kuziondoa.
viii. Ni jukumu la msingi la mwanafunzi kusoma kwa bidii na ni mwiko kwa mawanafunzi kupata alama chini ya 50% (asilimia hamsini ) kwa somo lolote.
ix. Ni kosa na ni marufuku kwa mwanafunzi kutembelea nyumba za watumishi bila sababu ya msingi na bila kupata kibali maalumu toka kwa Mkuu wa shule.
x. Ni jukumu la mwanafunzi kufuata ratiba zote za shule kiukamilifu sawasawa na ratiba ya siku ya shule inavyotaka bila kukosa.

**MUHIMU**

- Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.
- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yeyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.
- Mwanafunzi awapo shuleni anatakiwa kulala kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa na sio vinginevyo.
- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa au kibali maalum toka kwa Mkuu wa shule ( Msiba au ugonjwa)

**(B) MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

i. Wizi
ii. Kuto hudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa (utoro)
**iii. Kuondoka katika eneo la shule bila kibali cha Mkuu wa Shule/utoro.**
**iv. Kugoma na kuhamasisha mgomo**
v. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
vi. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi/kumpiga mwalimu au mtu yoyote Yule.
vii. Hauruhusiwi/na nikosa kusuka nywele kwa mtindo wowote ule.
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
ix. Uvutaji wa sigara na bangi
x. Uasharati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba ndani na nje ya shule,
xii. Kushiriki matendo ya uharifu, siasa na matendo yoyote yanayovunja sheria za nchi.
xiii. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi na viambata vyake vyovyote katika mazingira ya shule.
xv. Kudharau bendera ya Taifa.
**xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, kutishia kujiua au kuhatarisha maisha ya watu wengine.**
xvii. Uharibifu wa mali ya uma kwa makusudi.

**TANBIH**

Siku za hivi karibuni kumekuwa na wimbi kubwa la matapeli ( wizi kwa njia za mitandao). Baadhi ya wazazi wamejuwa wakitumiwa ujumbe mfupi na watu wanaojitambulisha kuwa ni walimu na kutoa taarifa kuwa watoto wao wako mahututi na hivyo watume pesa. Tafadhari usitume pesa yeyote, ni vema ukawasiliana na uongozi wa shule ili kupata ukweli wa taarifa husika kwa namba za simu zilitajwa hapo juu (Mkuu wa Shule na MAkamu wa Mkuu wa shule)

**MINISTRY OF EDUCATION SCIENCE TECHNOLOGY**
**TUNDURU DISTRICT COUNCIL**

**MASONYA GIRL'S SECONDARY SCHOOL**
P.O.BOX **159,**
**TUNDURU.**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.**

Please Examine Miss........................................................................................................ as her physical and mental fitness for admission as a form .................... student at MASONYA GIRL'S SECONDARY SCHOOL in the year.........................

Your sincerely

....................................

MAKRINA T. NGONYANI
HEADMISTRESS

**THE MEDICAL OFFICE**

................................................................

................................................................

................................................................

**STUDENTS' FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

**To be completed by a Medical Officer in respect of all pupils from this school**

1. Full pupils name ..............................................................................
2. Age ............................ (Years).....................................................
3. Food counts (Red and white) ..........................................................................................
4. Stool Examination .........................................................................
5. Urinalysis ......................................................................................
6. Syphilis tests .................................................................................
7. Venereal disease test ......................................................................
8. T.B Test..........................................................................................
9. Eye Test..........................................................................................
10. Ear ................................................................................................
11. Chest .............................................................................................
12. Spleen ...........................................................................................
13. Abdomen .......................................................................................
14. Urine for plan test ..........................................................................

**ADDITIONAL INFORMATION** (*If any*) e.g. Physical affects or impairment(s) arm, leg, Infections chronic family disease etc.

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

I certify that the mentioned above is fit/unfit to pursue educators as stated above.

Signature ..................................................
Designation ..............................................
Station ......................................................
Date .........................................................

# HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU

## FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI TEULE YA WASICHANA MASONYA

## A: SEHEMU YA MWANAFUNZI

1. Mimi.......................................................................................................ninakubali kujiunga Masonya sekondari Shule ya Wasichana ya Bweni kidato cha.................................mwaka..................................
2. Ninaahidi kufika shuleni tarehe .................................. iliyopangwa bila kuchelewa. Ninaahidi kwamba nitakuwa mwanafunzi bora mwenye bidii katika kujifunza na mtii kwa sheria za shule, walimu, walezi na viongozi wa shule kwa muda wote nitakapo kuwepo shuleni lakini pia ata nitakapo hitimu masomo.
3. Pia ninaahidi kutoshiriki katika migomo yeyote, kufanya fujo, au makosa yeyote ya jinai kwa kipindi chote nitakacho kuwa mwanafunzi nikiwa shuleni ama sehemu nyingine yeyote.

**SAINI ..........................................................  TAREHE ..........................................................**

**B: SEHEMU YA MZAZI/MLEZI**

1. Mimi.........................................................................ninakubali/sikubali mtoto wangu kujiunga na shule ya sekondari ya wasichana ya Masonya kuanzia tarehe ....................................
2. Ninaahidi kumpatia vitu vyote anavyotakiwa kufika navyo shuleni kama ilivyotajwa katika barua ya maagizo (Joining Instruction).
3. Ninaahidi kuwa nitaonyesha ushirikiano wa hari ya juu sana na kwamba sitamsumbua MKUU wa shule ikitokea **amenihitaji** kwa ajili ya **ugonjwa ama vyovyote** kuhusiana na mtoto wangu.
4. Nitahakikisha kwamba mtoto wangu amesoma sheria zote muhimu za shule na kuzielewa, na ameahidi mbele yangu kuwa atakuwa mtiifu na mwenye **BIDII** (**katika masomo ya darasani na elimu ya kujitegemea**)
5. Nina ahidi mtoto wangu hata jihusisha na migomo, fujo au vitendo vya uvunjifu wa amani awapo shuleni ikiwepo vitendo vya **WIZI**.
6. Awapo shuleni mtoto wangu alelewe katika dini ya ..........................................................................................
7. Anuani yangu ya kudumu ni:...........................................................................................................................
8. Namba za simu: ................................................................................................................................................
9. Majina ya NDUGU WATATU wakaribu walioidhinishwa kuchukua nafasi ya mzazi ikitokea dharura.

| Na. | Jina | uhusiano | anakoishi | Namba ya simu |
|---|---|---|---|---|
| 01 | | | | |
| 02 | | | | |
| 03 | | | | |

**SAINI.............................................................. TAREHE.......................................**

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU
SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA YA MASONYA
## TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina kamili ........................................................................................................tarehe ya kuzaliwa (......../......./20.......)

2. Kabila .................................................... Taifa ..........................................................................................

3. Dini ........................................................ Dhehebu ..................................................................................

4. Shule anayotoka mwanafunzi............................................. alama alizopata (wastani/div).......................

5. Jina la Baba ............................................................................. Taifa .................................anuani..........................................

6. Kazi ya Baba ............................................................................................... Simu na ....................................................

7. Jina la Mama ......................................................................... Taifa ..................................anuani..........................................

8. Kazi ya Mama ............................................................................................. Simu na ....................................................

9. Wazazi wanaishi Pamoja au wametengana...................................................................................................

10. Kama unaishi au kulelewa na mtu ambaye si mzazi.

(a) Jina la mlezi...............................................................uhusiano wako naye.......................................

anuani ya mlezi...................................................simu na....................................................................

11. Wakati wa likizo utakuwa kwa nani na wapi (Taja sehemu Moja tu utakayo kwenda kila wakati na anuani).

Nitakuwa kwa..................................................(wapi)................................................simu na..................

12. Hapa shule ningependa nijiunge na;

(a) Michezo- (i)....................................................... (ii)..........................................................

(b)Miradi- (i).........................................................(ii)..........................................................

12. Nathibitisha kwamba habari zote nilizotoa hapa ni kweli na sahihi.

Saini ya Mwanafunzi ....................................... (mbele ya mazazi/mlezi) Tarehe ...................................

Saini ya Mzazi/Mlezi ........................................(Baada ya mwanafunzi kusaini) Tarehe ..............................